# Learning by Ear 2010 – Urban Exodus – "Against the Current"

## Episode 05: "What's the point in being right if you're the only one?"

**Author: Alfred Dogbé**

**Editor: Yann Durand**

**Translator: Anne Thomas**

WAHUSIKA:

Onyesho la 1:

- **ZEINA** (UMRI MIAKA 24, MCHUMI, RAFIKI YAO BAKI NA BEN)
- **BEN** (MHANDISI WA KILIMO, UMRI MIAKA 29)
- **HADARI** (UMRI MIAKA 48, MKUU IDARA YA HUDUMA ZA MASHAMBANI)

Onyesho la 2:

- **BAKI** (UMRI MIAKA 26, MWANAELIMUJAMII, RAFIKI YA ZEINA NA BEN)
- **NANA** (UMRI MIAKA 22, MWENYEKITI WA CHAMA CHA VIJANA)
- **HADIA** (UMRI MIAKA 45, MAMA YAKE NANA)

Onyesho la 3:

- **BEN** (MHANDISI WA KILIMO, UMRI WA MIAKA 29)
- **KABO** (MKULIMA, MJOMBAKE BEN, UMRI MIAKA 57)
- **BAKI** (UMRI MIAKA 26, MWANAELIMUJAMII, RAFIKI YA ZEINA NA BEN)
- **ZEINA** (UMRI MIAKA 24, MCHUMI, RAFIKI YAO BAKI NA BEN)

## Intro:

Karibu kwenye *Learning by Ear* kipindi cha tano cha mfululizo wetu kuhusu uhamiaji mijini uitwao “Kukabiliana na Wimbi la Mabadiliko”. Ben, Baki na Zeina, ambao hawana ajira na walio na shahada za chuo kikuu, wanaamua kuondoka mjini kutokana na ukosefu wa ajira. Wanataka kuanzisha chama cha ushirika cha ukulima kijijini. Wanakijiji wana hamu ya kujua hasa kilichowafanya vijana hao watatu kurejea kijijini.

Wakati huo huo, Zeina na Baki, ambao wanapendana, hawaeleweki: Baki anataka kuhamia Marekani, ilhali Zeina anahisi kwamba kijijini ndiko wanakofaa kuishi.

Katika kipindi hiki cha tano,utagundua kuwa hatua ya kuanzishwa chama cha ushirika inaibua mambo yasiyotarajiwa.

| Scene 1: Village bar.<br>BEN, ZEINA, HADARI. |
|---|

1. **SFX: VILLAGE BAR. CONVERSATIONS, LAUGHTER, DANCE MUSIC IN THE BACKGROUND.**

2. **ZEINA** Bwana Hadari?

3. **HADARI** Naam, mimi hapa. Naomba nicheze densi nawe kidogo?

4. **ZEINA** La, asante… Hujambo. Jina langu ni Zeina, mimi ni

mwanauchumi.

5. **BEN** Na mimi ninaitwa Ben. Mtaalamu wa Kilimo. Tungependa kushauriana nawe ikiwa una nafasi.

6. **HADARI** Alaa! Watu wamekuwa wakizungumzia chama chenu cha ushirika tangu wiki mbili zilizopita wala hamjataka kukutana nami. Sielewi! Mimi ndiye mkuu wa huduma za maendeleo ya mashambani hapa. Ninawakilisha serikali!

7. **ZEINA** Kweli hilo. Tulikuja afisini kwako mara tatu kwa lengo la kukutana nawe.

8. **BEN** Hukuwepo mara mbili za kwanza.

9. **HADARI** Nilikuwa nyanjani. Mngeniandikia barua. Hivyo ndivyo kazi inavyofanywa.

10. **BEN** Tuliona bora tukutane nawe kabla ya kukuandikia barua.

11. **HADARI** Hapa si mahala panapofaa na huu si wakati mwafaka. Ninapokuja hapa, mimi huja kujiburudisha. Siji kufanya kazi.

12. **BEN** Kweli unayosema. Lakini tungependa kuwa na mazungumzo yasiyo rasmi.

13. **ZEINA** Tulitaraji utajiunga nasi kwa kinywaji. Ili tufahamiane vizuri.

14. **HADARI** Mmm… Sawa. Wazo zuri hilo! Mhudumu! Tuletee kinywaji, bia… marafiki zangu watalipa.

15. **SFX: THREE CHAIRS BEING PULLED OUT AND ADJUSTED**

**16.** **HADARI** Naam, nambieni niwasaidie vipi?

**17.** **BEN** Tungependa kuanzisha chama cha ushirika cha ukulima ambacho kitawapa wanakijiji huduma za kiufundi ili kuimairisha ukuzaji na uuzaji wa mazao yao.

**18.** **HADARI** Mnataka kuifanya kazi yangu?

**19.** **BEN** Kwa namna fulani ndiyo… Lakini hatutafuata mwelekeo sawa.

**20.** **ZEINA** Tunadhamiria kuongeza na kuimarisha mazao ya kilimo kwa manufaa ya wakulima.

**21.** **HADARI** Nani anahusika na yote hayo?

**22.** **BEN** Sijakuelewa.

**23.** **HADARI** Nani anafadhili shirika lenu hilo lisilo la kiserikali?

**24.** **BEN** Ni chama cha ushirika...

**25.** **HADARI** ... ambacho hakifadhiliwi na umma na kwa hivyo ni shirika lisilo la kiserikali.

**26.** **ZEINA** Kweli.

**27.** **HADARI** Ikiwa serikali haijakifadhili chama chenu, basi nani anayekifadhili?

**28.** **BEN** Tumechanga fedha zetu wenyewe.

**29.** **HADARI** Hamna mfadhili kutoka nje?

**30. BEN** Hapana!

**31. HADARI** Kweli? Inawezekana?

**32. ZEINA** Tumeamua kufuata mwelekeo wa kiuchumi wa kijamii ambao unaendeleza umoja. Mwelekeo huo unazingatia jinsi watu wanavyojitolea na matumaini yao kuafikia malengo yao kwa ushirikiano-hizo ndizo rasilimali zetu.

**33. SFX: BOTTLES AND GLASSES BEING PUT ON A TABLE. LIQUID BEING POURED INTO THE GLASSES**

**34. HADARI** Hatimaye vinywaji hivi vimeshaletwa. Natumai bia yenyewe ni baridi!

(**DRINKS LOUDLY AND PUTS HIS GLASS ON THE TABLE**)

Aha! Ni baridi! Basi mnataka nini kwangu?

**35. BEN** Wewe ndiye mwakilishi wa mamlaka ya usimamizi na tunajua uzoefu wako wa nyanjani utatufaidi kwa kiasi kikubwa.

**36. HADARI** Mara nyingi, watu huja hapa na magari yao makubwa ya kifahari. Wanadhani wanaweza kutelekeza jambo lolote bila kuihusisha idara yangu. Mimi huwatazama wakijihangaisha hadi pale wanapotambua umuhimu wa idara yangu.

**37. BEN** Ndiyo hivyo. Ndiposa tunataka msaada wako.

**38. HADARI** Hilo si tatizo. Idara yetu ni idara ya umma maanake tunawahudumia wateja wetu wote. Ingawa tuna rasilimali chache, jukumu letu ni muhimu sana. Unajua… Nimeshuhudia mambo mengi… Bila mimi… vyote unavyoviona…

**----- MUSIC -----**

**Scene 2: Nana's home. Early evening.**
**HADIA, BAKI AND NANA.**

**39. SFX: NANA'S HOME. EARLY EVENING. CRICKETS, KITCHEN NOISES**

**40. BAKI** Haya, Shangazi Hadia, asante sana. Sina budi kutenda wanayoyatenda wageni wote, yaani kuondoka…

**41. HADIA** Wewe si mgeni hapa.

**42. BAKI** Bila shaka mimi si mgeni. Ulimi umenicheza, shangazi!

**43. NANA** Ma, tunaondoka. Kuna watu wengine wawili tunaotaka kushauriana nao.

**44. HADIA** Sawa! Kila la heri! Nitaendelea kuwafahamisha marafiki zangu kuhusu mradi. Natoa ahadi hiyo. Hasa ikiwa mtaendelea kuwa pamoja. Mnapendeza sana mnapokuwa wawili!

**45. NANA** Unakusudia nini, ma?

**46. HADIA** Ingawa nimezeeka mimi si kipofu!

**47. NANA** Hutawahi kubadilika!

**48. HADIA** Kweli unayosema! Nilipokuwa mdogo nilibandikwa jina la "mpatanishi". Nilikuwa nikiwakutanisha watu na pia kuwapatanisha wanapogombana. Wale ambao sikuwa nikipatana nao walijihadhari sana nami! Nilijua jinsi ya kuunganisha na pia jinsi ya kutenganisha!

**49. NANA** Baki twende zetu!

**50. SFX: SOUND OF STEPS – IRON GATE OPENING AND GRATING**

**51. HADIA** Muwe waadilifu!

**Scene 3: At Ben's**

**BEN, ZEINA, BAKI AND KABO.**

**52. SFX: AT BEN'S. MURMURING IN THE BACKGROUND**

**53. BEN** Tumezungumzia shabaha na malengo yetu, mkakati wetu na majukumu makuu ya chama cha ushirika. Hata hivyo inatubidi tukubaliane kuhusu usimamizi na jinsi chama chenyewe kitakavyoendeshwa. Baki ana mapendekezo. Ebu tueleze.

**54. BAKI** Ninapendekeza mambo yafuatayo katika chama chetu: kama kuu, wanachama, kitengo cha usimamizi, tume ya kufuatiliza na makundi ya utekelezaji.

**55. ZEINA** Kitengo cha usimamizi unapendekeza kiwe vipi?

**56. BAKI** Afisi ya utendaji ijumuishe mkuu, katibu wa utawala pamoja na fedha, katibu atakayesimamia masuala ya nje, na katibu wa kuratibu shughuli za chama.

**57. BEN** Napendekeza badala ya kutumia “katibu” tubadilishe iwe “mkurugenzi”. Hili lina uzito zaidi.

**58. BAKI** Sawa… Kitengo cha wasimamizi kitajumuisha Afisa Mkuu Mtendaji, mkurugenzi msimamizi na wakurugenzi watatu maalumu. Wote kwa jumla ni watano. Nadhani hao wanatosha, ama vipi?

**59. ZEINA** Naam, vizuri hivyo. Wakiwa wengine kazi haitendeki vyema.

**60. BEN** Pia inalingana na hali yetu tulivyo. Sote hapa tunaweza kujumuishwa kwenye kitengo cha usimamizi.

**61. BAKI** Jukumu la kitengo cha usimamizi ni kukiwakilisha chama, kuongoza na kusimamia shughuli zake, pamoja na uhusiano na wafanyikazi, maanake kitengo hicho hupanga, huongoza na kuratibu chama.

**62. ZEINA** Kwa hivyo tunatakiwa kubainisha majukumu ambayo kila mmoja wetu anapaswa kuyatwaa.

**63. BAKI** Bila shaka. Wanachama wote wanapaswa kukubali jinsi nyadhifa zitakavyogawanywa.

**64. KABO** Na vipi mtakavyogawana kazi na majukumu baina yenu?

**65. BAKI** Napendekeza Ben awe mkurugenzi msimamizi. Yeye ni mtaalamu wa kilimo na ameshawahi kuwa msimamizi wa mradi alipokuwa akifanya kazi wizarani. Yeye ndiye aliyetoa fikra ya kutuunganisha kuanzisha chama.

**66. SFX: LOUD APPLAUSE**

**67. BEN** Mjomba Kabo, ungetaka kuwa Afisa Mkuu Mtendaji?

**68. KABO** Cheo chenyewe kinahusu nini?

**69. BEN** Afisa Mkuu Mtendaji huwakilisha shirika katika jamii. Ili chama kifanikiwe inabidi kuzingatia jinsi wawakilishi wake wanavyopokelewa kokote wanakokwenda. Watu wanakuheshimu. Ukiwa mkuu wa chama watu wote watakitilia maanani.

**70. ZEINA** Afisa Mkuu Mtendaji pia huhakikisha kwamba shirika lina umoja. Kazi yako kama ya baba, na umekuwa hivyo kwetu sisi kila mara. Utalipokea jukumu hili ili uongoze shughuli baina yetu sisi na pia baina ya wanakijiji na sisi.

**71. KABO** Kweli, mimi kama mjomba wenu. Lakini ni mkulima wa kawaida. Sina ujuzi mlio nao, wala sina fedha ambazo chama kinahitaji.

**72. BAKI** Chama chetu kitazingatia demokrasia. Hakihitaji kiongozi anayejua kila jambo na anayeweza kufanya kila jambo.

**73. BEN** Jukumu lako ni kutuongoza tusikiuke shabaha na malengo yetu pamoja na msingi ambao chama hiki kimeundiwa

**74. ZEINA** Kiongozi pia ana majukumu ya kisheria. Yeye ndiye atakayekiwakilisha chama kwenye masuala ya kisheria.

**75. KABO** Hii ni kazi ngumu kweli! Niombeeni Mungu nipate kufanikiwa.

**76. SFX : (CLAPPING AND CRIES OF JOY)**

**77. KABO** Hata hivyo tunajuaje iwapo wanachama wa baadaye watakubali?

**78. BAKI** Tutapendekeza kitengo cha muda cha usimamizi katika mkutano wa kwanza wa baraza kuu. Kusema kweli wanachama hawatapata watu wengine wa kuwachagua.

**79. BEN** Una maana gani?

**80. BAKI** Sisi waasisi tutawaalika wakazi kwenye mkutano wa baraza kikuu. Iwapo watakuja ni dalili kwamba wanakubaliana na mapendekezo yetu. Tunatakikana tuwe wakweli na kuwaelezea kila kitu kwenye kikao hicho na hata baadaye.

**81. ZEINA** Tusipofanya hivyo huenda chama hatimaye kikaendeshwa na watu wasio kuwa na misimamo sawa na yetu.

**82. BAKI** Wasiokubaliana nasi watakuwa na uamuzi mmoja tu – hawatakubali kuwa wanachama. Basi.

**83. KABO** Sawa, ninakubali!

**84. SFX : (CLAPS AND CRIES OF JOY)**

**85. BAKI** Vyema! Nyadhifa nyingine napendekeza ziwe hivi. Mkurugenzi Msimamizi: Ben. Utawala: Zeina. Uzalishaji: mimi. Uratibu: Nana.

**86. BEN** Nadhani ana sifa hizo. Mafunzo yake ya mawasiliano pamoja na jinsi anavyojihusisha na maisha ya kijijini ni sifa muhimu sana…

**87. KABO** Tena ni msichana mzuri.

**88. ZEINA** Natumai atakubali. Kuna mtu kamweleza?

**89. BAKI** Bado.

**90. BEN** Kwanza tukubaliane baina yetu kabla ya kwenda kumjulisha. Mimi nakubali.

**91. ZEINA** Mimi pia.

**92. KABO** Mimi pia. Ninajua amekuwa akikitetea chama hiki.

**93. BAKI** Ben, wewe ndiye utakayemwarifu uamuzi wetu.

**94. BEN** Si bora zaidi Mjomba Kabo afanye hivyo?

**95. ZEINA** Hapana. Uajiri ni moja wapo ya majukumu ya mkurugenzi msimamizi. La muhimu tu ni kwamba kundi lote linalohusika linakubaliana na hatua ya zinazochukuliwa.

**96. BAKI** Kweli hayo.

**97. BEN** Sawa, nitafanya hivyo.

**98. KABO** Nadhani tuko tayari. Tunaweza sasa kupanga tarehe ya

mkutano mkuu. Juma lijalo?

**99. EVERYBODY**

Sawa ! **(followed by conversations etc….)**

**Outro:**

Mwisho wa kipindi cha *Learning by Ear* cha leo. Tunakushukuru kwa kufuatilia kipindi cha tano cha "Kukabiliana na Wimbi la Mabadiliko", mfululizo wa michezo ya redio kuhusu uhamiaji mijini.

Ungependa kujua endapo wanakijiji watajiunga na mradi wa Ben na marafiki zake? Basi, usikose kutegea sikio kipindi kijacho.

Ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki au kutupatia maoni yako, fungua ukurasa wetu wa tovuti www.dw-world.de/lbe au utuandikie barua-pepe kupitia anwani lbe@dw-world.de.

Kumbuka kusikiliza kipindi kinachofuata!

**END OF EPISODE 5**